



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA

UDIWANI KATIKA KATA MBILI (02) ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ambaye kwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata za **Mwanahina** katika Halmashauri ya Wilaya ya **Meatu** Mkoani Simiyu na Kata ya **Biturana** katika Halmashauri ya Wilaya ya **Kibondo** Mkoani Kigoma. Nafasi hizo wazi zimetokana na kujiuzulu uanachama.

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa Umma kuhusu uwepo wa Uchaguzi mdogo wa Udiwani katika Kata tajwa zilizopo katika Halmashauri za Meatu na Kibondo. Tume imepanga kuendesha Uchaguzi huo Mdogo wa Udiwani katika Kata hizo kwa kuzingatia Ratiba ifuatayo:

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe 21 hadi tarehe 27, Disemba mwaka huu.

2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 27, Disemba mwaka huu.
3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 28, Disemba mwaka huu hadi tarehe 18 Januari 2019 na,
4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe 19 Januari 2019.

Uchaguzi wa Kata hizo utafanyika pamoja na uchaguzi wa Jimbo la Temeke na Kata 46 za Tanzania Bara, kama ilivyotangazwa hapo awali.

Tume inapenda kuvikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha Uchaguzi huu mdogo.

Imetolewa leo tarehe 18 Disemba, 2018.

Jaji (Rufaa) Mbarouk Salim Mbarouk

MAKAMU MWENYEKITI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI